JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S.L.P 1951, Moshi-Kilimanjaro

Simu: 027-2750885; Nukushi:027- 2750889

Barua pepe: rbckilimanjaro@pccb.go.tz

Wavuti: www.pccb.go.tz

KILIMANJARO – APRILI 23, 2020

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

TAKUKURU YATAHADHARIASHA MIRADI YA AFYA, MAJI NA SHULE ISIFANYIWE UBADHIRIFU.

TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro inafanya uchunguzi wa ubadhirifu wa fedha shs. 960,994,000 za malipo hewa ya vifaa vya miradi ya maji na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Siha, uhamisho wa walimu, fedha za kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura pamoja na fedha za kujikimu za masaa ya ziada kwa watumishi mbali mbali wa Idara ya Afya Wilayani Siha.

Hivyo kutokana na uchunguzi huo, TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro inawatahadharisha na inawaonya watumishi na wakandarasi wanaohusika na kutekelezaji wa miradi ya maji, ujenzi wa hospitali, vituo vya afya, zahanati, shule - mabweni na miradi mingine inayoendelea katika Mkoa wa Kilimanjaro, kufanya kazi hizo kwa weledi, kwa wakati na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili miradi husika iweze kukamilika ikiwa inalingana na thamani halisi ya fedha zilizotolewa (value for maney).

TAARIFA ZILIZOPOKELEWA

Katika kipindi hiki cha miezi mitatu (Januari – Machi 2020) tulipokea taarifa 151, kati ya hizo zilizoonekana kuwa za makosa ya rushwa ni 110 na ambazo hazina uhusiano na makosa ya rushwa ni 41. Mchanganuo wa taarifa hizo kisekta ni Elimu 22, Serikali za Mitaa 21, Polisi 10, Sekta Binafsi 10, Mahakama 7, Ardhi 14, Afya 17, Vyama vya Ushirika 16, Madini 1, Utalii 1, Uchaguzi 1, Mashirika ya Umma 1, Maji 3, Bima 1, Mifuko ya Mafao 3, TRA 1, Uhamiaji 2, Halmashauri 15 na Ulinzi 5.

Taarifa zote za makosa ya Rushwa zimefanyiwa kazi na uchunguzi upo katika hatua mbalimbali za kiutawala.

MASHTAKA

Mashauri mapya yaliyofikishwa mahakamani ni **02** ambayo ni kama yafuatavyo:-

CC.38/2020 inayomhusu **Wilbert Joseph Mayila** ambaye ni afisa mpima ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Kesi hii ipo Mahakama ya Wilaya Hai na

CC.141/2020 inayomhusu **Benedict Kimaro** ambaye ni Mshauri wa Mahakama ya Mwanzo Moshi. Kesi hii ipo katika Mahakama ya Wilaya ya Moshi.

Mashauri yaliyokamilika ni manne (4) ambapo tulishinda matatu **(03)** na kushindwa moja **(01)**

Mashauri tuliyoshinda ni

CC 403/2018; JAMHURI DHIDI YA GASPER MSUYA

Huyu, alituhumiwa kwa makosa ya kuomba na kupokea rushwa ya shilingi 50,000.00 (hamsini alfu) kutoka kwa mlalamikaji ili ampatie nakala ya hukumu ya shauri la baraza la ardhi kata ya njia panda. Alihukumiwa kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya shilingi 500,000.00(laki tano) kwa kila kosa. Alilipa shilingi 1,000,000.00(milioni moja) na kuwa huru,

CC 52/2019; JAMHURI DHIDI YA SOLOMON KILEO

Solomon Kileo – alikuwa ni mlinzi wa Mahakama ya Mwanzo Moshi ambaye alishtakiwa kwa kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu baada ya kujifanya ni Afisa wa RITA na alimtaka mlalamikaji ampatie kiasi cha shilingi 40,000.00 (arobaini alfu) ili amsaidie kupata cheti cha kuzaliwa na alitiwa hatiani na kutakiwa kulipa faini shilingi 200,000.00 (laki mbili) au kwenda jela miezi miwili, na

CC 70/2019; JAMHURI DHIDI YA RAYMOND MSUYA

Huyu alikuwa ni Askari wa Jeshi la Akiba katika mji mdogo wa Same - **RAYMOND MSUYA** ambaye alishtakiwa kwa kuomba na kupokea rushwa ya shilingi 20,000.00 kutoka kwa Osmunda Joseph ili amsaidie asichukuliwe hatua kwa kufuga nguruwe katika makazi ya watu na alitiwa hatiani kwa makosa yote mawili na kutakiwa kulipa faini ya shilingi 600.000.00 (laki sita) kila kosa iliyofanya jumla ya shilingi 1,200,000.00 au kifungo jela miaka 3.

Shauri tuliloshindwa ni CC 20/2018; JAMHURI DHIDI YA HUMPHREY KIRUMBUYO iliyomhusu **HUMPHREY KIRUMBUYO** ambaye ni Mwalimu Mkuu katika shule ya sekondari Kishisha aliyeshitakiwa kwa Matumizi mabaya ya fedha za sekondari kishisha wilayani Siha. Ameachiwa huru.

FEDHA ZILIZOOKOLEWA

Jumla ya **shs. 33, 212, 500/= (milioni thelathini na tatu laki mbili kumi na mbili alfu mia tano tu)** ziliokolewa katika kipindi cha Januari – Machi, 2020 ambapo

- **shs. 11,500,000/= (milioni kumi na moja laki tano tu)** zilirudishwa na SHEDEWA ENTERPRISES & LOGISTICS aliyesambaza vitasa duni katika mradi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Siha uliofuatiliwa na TAKUKURU.
- **shs. 4,990,000/= (milioni nne, laki tisa tisini alfu)** zilirudishwa na **CHRISTOPHER KUNIBERT NGONYANI mlinzi katika shamba la West Kilimanjaro** aliyejipatia fedha hizo kwa njia za udanganyifu kutoka kwa walinzi wenzake kwa kuwatoza shs 10,000.00 kila walipoenda mapumziko kwa madai kuwa zinatumika kulipa walinzi wa muda pale wanapokuwa mapumziko au likizo. Fedha hizo walikabidhiwa wahusika.
- **shs. 2,159,000/=(milioni mbili laki moja hamsini na tisa alfu)** zilirudishwa na **PERE MUGANDA, NAMSON FISSO na FRANK BAHATI** pesa zilizofujwa katika uhamisho wa watumishi, uboreshaji wa daftari la wapiga kura, manunuzi ya vifaa vya ujenzi wa hospitali ya

Wilaya Siha na Mradi wa EGPAF.

- **shs. 300,000/=(laki tatu)** zilirudishwa na **NATHANIEL MNDEME** ambaye alilipwa fedha hiyo mara mbili katika **ujenzi wa hospitali ya Wilaya Siha ili awalipe vibarua.**
- **shs 1,000,000/= (milioni moja)** ilirejeshwa na waliokuwa Viongozi wa Chama cha Malida SACCOS Rombo, fedha ambayo ilichukuliwa kinyume cha sheria na utaratibu. Fedha hiyo itakabidhiwa Malida SACCOS.
- **shs 963,500/=(laki tisa sitini na tatu alfu mia tano)** zililipwa kwa wakulima, fedha ambayo ilikuwa ni marejesho kutoka kwa wajumbe wa kamati ya pembejeo na wakala, msimu wa 2010/11 wilayani Mwanga ambayo wakulima hao walidhulumiwa.
- **shs 9,600,000/=(milioni tisa laki sita)** zilirejeshwa wilayani Hai na Bw. Spouse Mushi kama kodi kwa kipindi chote alichojimilikisha eneo la TANESCO na kukabidhiwa kwa TANESCO.
- **shs 2,200,000/=(milioni mbili laki mbili)** zilirejeshwa na Peter Orota Afisa Mikopo wa Kindi SACCOS Moshi na kukabidhiwa kwa wanachama wawili waliochukuliwa fedha zao na afisa huyo baada ya afisa huyo kuwaelekeza kumdhamini mtu wasiyemjua na mtu huyo kutoweka na
- **shs 500,000/=(laki tano)** zilirejeshwa kutoka kwa aliyekuwa mhasibu wa Uru Mashariki SACCOS Moshi Bw. Innocent Massawe aliyezichukua kinyume na utaratibu.

UZUIAJI RUSHWA

Uchambuzi wa Mifumo

- Uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa vyama vya ushirika katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi vijijini ulifanyika na tathmini inaonesha kuwa uendeshaji wa vyama vya ushirika una mapungufu mengi yakiwemo viongozi wasiofaa, uwekaji mbovu wa kumbukumbu na ubadhirifu hali inayopelekea vyama vingi kuwa ni vyama mfu. Mrajis kwa kushirikiana na COASCO wanapaswa kusimamia na kudhibiti vyama vya ushirika ili kupunguza au kuondoa kabisa changamoto hizo. Warsha kwa ajili ya kuweka maazimio ya kutatua changamoto hizo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio utaendelea.
- Pia ulifanyika uchambuzi katika mfumo wa usimamizi na udhibiti hifadhi za wanyamapori na maliasili na ikabainika kuwa kuna changamoto nyingi zikiwemo za askari misitu wasio waadilifu, namna duni ya ukusanyaji mapato, uhaba wa wataalamu wa uhifadhi wa misitu na maliasili na elimu duni kwa wananchi katika uhifadhi misitu na maliasili.

  Mhifadhi wa misitu kutoka katika ofisi ya Wakala wa huduma za misitu (TFS) kwa kushirikiana na Afisa maliasili wa Mkoa wanapaswa kuongeza jitihada za kusimamia na kuhifadhi misitu na maliasili ikiwa ni pamoja na kupanga mikakati thabiti ya kukusanya mapato, kupambana na rushwa na kuwawajibisha askari wasio waadilifu

Ufuatiliaji wa Rasilimali za Umma

- Wilayani ya Siha TAKUKURU ilikagua miradi miwili ya maendeleo katika kata ya Songu na kata ya Orkolili ambapo ilikagua miradi ya maendeleo ya ujenzi wa madarasa, maabara na vyoo yenye **thamani ya shs. 492,746,279/=,** Fedha zilizotumika katika miradi yote miwili ni kiasi cha **shs.113,388,000/=** ambapo katika miradi hii miwili kuna thamani halisi ya fedha (**VALUE FOR MONEY),** ingawa taratibu za manunuzi kwa utaratibu wa FORCE ACCOUNT hazikuzingatiwa na ushauri umetolewa kwa wasimamizi wa miradi hii wazingatie taratibu za manunuzi na zaidi wajumbe wa kamati za ujenzi katika shule zote mbili wataelimishwa mara baada ya ugonjwa wa CORONA kupita.
- Huko Holili TAKUKURU imefuatilia jumla ya miradi mitatu yenye thamani ya shs 381,382,500/- (milioni mia tatu themanini na moja laki tatu themanini na mbili alfu mia tano) ambayo ni ukarabati na upanuzi wa barabara katika kata ya mwika, mamba kaskazini, kilema na marangu magharibi (Kiracha-Matala Komela zinazoungana takriban na barabara 7 feeder roads) wenye gharama ya shs.126,382,500/-(milioni mia moja ishirini na sita laki tatu themanini na mbili alfu mia tano) na miradi ya nyumba za walimu katika shule za Msingi Rauya wenye thamani ya Tshs 34,000,000/- (Milioni Thelathini na nne) na Marimeni wenye thamani ya shs 121,000,000/- (Milioni mia moja ishirini na moja) ambayo michakato ya ufuatiliaji nyaraka unaendelea.
- TAKUKURU (W) Mwanga imefuatilia mradi wa ujenzi wa bwalo la wanafunzi katika shule ya sekondari Kamwala wenye thamani ya shs 100,000,000 (milioni mia moja) ambapo ujenzi wake unaendelea vizuri japokuwa ilibainika kuwepo kwa changamoto za kuchelewa kusainiwa

kwa mkataba kati ya Halmashauri na Fundi, ubovu wa barabara unaosababisha kipindi cha mvua kushindwa kupitika kwa ajili ya kupeleka vifaa vya ujenzi, Kwa changamoto hiyo hiyo ya barabara kunapelekea kuongezeka kwa gharama za ujenzi na Umbali wa shule kutokea maeneo ya upatikanaji wa vifaa vya ujenzi zinazochangia katika ukamilishaji wa mradi.

- Ufuatiliaji wa mradi wa ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Moshi ambao ulipatiwa jumla ya shs 334.5M mwaka 2017 na una thamani ya zaidi ya shs 392.4 umezaa matunda kwani huo umekamilika na kukidhi vigezo na ofisi hiyo ya mkuu wa Wilaya imeanza kutumika kwa sasa.

ELIMU KWA UMMA

Katika kipindi hicho cha januari – machi 2020, tumefanya semina 27 kwa makundi mbalimbali, mikutano ya hadhara 44, uimarishaji wa Klabu za wapinga rushwa 95, tumeendesha vipindi vya radio 3, tumeshiriki katika maonesho 10 na tulitayarisha makala 12 kwa ajili ya machapisho yanayoandaliwa na TAKUKURU.

Elimu hii imeongeza uungwaji mkono kutoka kwa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa na hivyo kuwepo kwa taarifa nyingi za rushwa zilizopokelewa kama ilivyoelezwa hapo juu.

MWELEKEO WA APRILI - JUNI 2020

Nguvu itaelekezwa katika ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo hususan afya, rushwa katika uchaguzi ndani na nje ya vyama vya siasa ikiwa ni pamoja na uelimishaji wa mapambano dhidi ya rushwa katika kuelekea uchaguzi

mkuu ujao wa madiwani, wabunge na Rais. Tunaomba wananchi waendelee kutoa ushirikiano.

Imetolewa na:

Moses Oguda
K.n.y
Mkuu wa TAKUKURU (M) Kilimanjaro